



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 22nd April, 2025

**Third Assembly – Fourth Session
THIRTEENTH SITTING**

*[The County Assembly met at 11:26a.m at the County Assembly Buildings]
[The Deputy Speaker (Honourable Fadhili Mwalimu Makarani) in the Chair]*

PRAYERS

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Have your seat Members?

[Loud consultations]

PAPERS

QUARTERLY REPORT FOR FINANCIAL YEAR 2024/2025 FOR MOMBASA INVESTMENT
CORPORATION

Yes, Honourable Kibwana Swaleh Baya?

Oh! Sorry, the Deputy Majority Leader, Honourable Maimuna?

The Deputy Majority Leader (Hon. Maimuna Salim): Thank you, Mr. Speaker Sir, I stand to lay the Paper, Paper on quarterly report; quarter three (Q3) for Financial Year 2024/2025 for Mombasa Investment Corporation. I lay the Paper.

[Paper laid]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Members, the quarterly Report, quarter three (Q3) for Financial Year 2024/2025 for Mombasa Investment Corporation stands committed to the Committee on Trade, Tourism and Culture for consideration. Yes, Clerk?

REPORT ON THE PUBLIC PARTICIPATION OF THE MOMBASA COUNTY ANNUAL DEVELOPMENT PLAN
2025/2026

Yes, Honourable Kibwana Swaleh?

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Honourable Speaker. Honourable Speaker, I wish to lay the Paper on the Report on the public participation for the Mombasa County Annual Development Plan 2025/2026. Thank you, Honourable Speaker.

[Paper laid]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes Clerk?

NOTICE OF MOTION

ADOPTION OF REPORT ON PUBLIC PARTICIPATION OF THE MOMBASA COUNTY ANNUAL
DEVELOPMENT PLAN 2025/2026

Yes, Honourable Kibwana Swaleh Baya?

Hon. Kibwana Swaleh: Thank you Honourable Speaker. Honourable Speaker, allow me to give Notice of Motion on Adoption of Report on public participation for the Mombasa County Annual Development Plan 2025/2026. Mr. Speaker Sir, I beg to issue Notice of the following Motion;

That this House adopts the Report of the public participation on the Mombasa County Annual Development Plan, 2025/2026 as laid on the Table on Tuesday 22nd April, 2025.

Thank you, Honourable Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes Clerk?

MOTION

ADOPTION OF REPORT ON DRAFT LOCAL, PHYSICAL, AND LAND USE DEVELOPMENT PLAN FOR
KIKAMBALA, KISIMANI KWA NDEGWA, KIDUNGUNI, KIBUNDANI AND BASRA INFORMAL
SETTLEMENTS 2024/2034

Yes, Honourable Ahmed Khamis, the Vice Chair Committee on Lands and Urban Planning. Honourable Ahmed Khamis?

Hon. Ahmed Khamis: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir I beg to move the following Motion;

THAT this House adopts the Report on draft local physical and land use development plan for Kikambala, Kisimani Kwa Ndegwa, Kidunguni, Kibundani and Basra informal settlements 2024/2034 as laid on the Table on Tuesday 15th April, 2025 during the 11th Sitting.

Mr. Speaker Sir, I beg Honourable Madialo to second.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Yes, Honourable Madialo?

Hon. Madialo: Thank you Mr. Speaker Sir, I stand to second.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Members, I now propose a question that the Motion as moved by Honourable Ahmed Khamis on the draft Report on local, physical and land use development plan for the Kikambala, Kisimani Kwa Ndegwa, Kidunguni, Kibundani and Basra informal settlement 2024/2025 be debated in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Ahmed Khamis please build your Motion?

Hon. Ahmed Khamis: Thank you Mr. Speaker, recommendations are as follows;

- 1) Infrastructure development to prioritize upgrading roads, drainage system and sanitation facilities, to improve accessibility and living conditions, expand water supply system and integrate sustainable solutions like rainwater harvesting and sewer connections.
- 2) Tenure security, accelerate the process of land tenure regularization by issuing legal ownership documents to residents, explore joint or block titles to accommodate high-density settlements.
- 3) Economic empowerment, establish local market and vocational training programs to boost employment opportunities and income levels, to promote small and medium-sized enterprises, SMEs and support women, youth and persons with disabilities through financial education and access to credit.
- 4) Environmental management to develop community-based solid waste management initiatives including recycling, contacts and awareness campaign on proper waste disposal, to construct storm water drainage systems to mitigate flooding and prevent soil erosion.
- 5) Social infrastructure to construct dispensaries and early childhood development centers within settlements to improve access to health care and education, to use undeveloped spaces for additional public facilities such as recreational areas of schools.
- 6) Energy access to promote renewable energy solutions like solar power and LAPG and subsidies access for low-income households, to implement community awareness programs to encourage the adoption of clean energy technologies.
- 7) Transportation improvements to develop a phased approach to road expansion and upgrades while minimizing displacements, to enhance connectivity through integrated transportation plans linking settlements to key urban centers.
- 8) Governance and capacity building to strengthen local governance frameworks by developing policies for slum upgrading and disaster management, to foster collaboration between county government community groups and stakeholders for sustainable development efforts.

In conclusion, the Committee on Lands, Urban Planning and Housing recommends that this County Assembly adopts the Report of Committee on Lands, Urban Planning and Housing on the draft local physical and land use development plan Report for Kikambala, Kisimani Kwa Ndegwa, Kidunguni, Kibundani and Basra informal settlement 2024-2034. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you.

[Applause]

Honourable Prischillah?

The Majority Chief Whip (Hon. Mumba): Ahsante Mheshimiwa Spika. Nimesimama hapa kuunga mkono Kamati ya Ardhi na kuipa kongole kwa kutupa Ripoti na mapendekezo ambayo yatakayosaidia katika mabadiliko ambayo yatakikana yajitokeze na haswa sana kilicho nifurahisha katika Ripoti hii nimeangalia kwanza kwa *tenure security* ambayo watu katika hii Kaunti ya Mombasa ambayo ni namba mbili tunakuwa tuna hatari kubwa ya watu kupoteza rasilmali zao kwa sababu ya kuwa watu hawana stakabadhi muhimu za kuweza kukinga ardhi zao na kuweza kujielewa kuwa hapa ni kwetu ama si kwetu. Wakipata zile stakabadhi, itakuwa imeashiria kuwa watakuwa wana uhakika na pale mahali watakapo kuwa wanakaa kwa sababu shida kubwa ambayo tuko nayo Kaunti ya Mombasa, ni kutokuwa na makaazi ya wananchi na donda hilo sugu limetutatiza hata sisi viongozi kwa sababu wakati bwenyenye anapotaka kufanya mradi wowote, anaanza kugusa hawa wanyonge na kwa sababu hawana stakabadhi. Basi inakuwa na rahisi wao kuondolewa na wanatulilia sisi kama viongozi wa chini ambao tuweze tuone vile tutawasaidia.

Lengine ni hata kwa upande wa mwangaza, ama usalama hiyo *infrastructure* barabara vile itakavyo kuwa inapangwa; hizo miundo misingi ya maji taka kama wakati huu ni wakati wa mvua na wakati huu kutakuwa na *blockages* nyingi sana za maji ambazo zitakuwa zinakithiri katika barabara zetu na majumba yetu hata nyengine huwa zinafurika na kuzama na tunapata maafa mengi na tunapata matatizo mengi kwa sababu Kaunti ya Mombasa muundo msingi ambao uko katika hizi sehemu ambazo tunasema ni vitongoji watu wamejenga wamejifinyilia kupita kiasi hata wakati Serikali ya Kaunti inataka kupeleka gari za wazima moto kama kumetokea majanga inakuwa ni shida kupita. Haya mambo yote ambayo yamenukuliwa yatarahisisha muundo msingi mambo ya kisasa ambapo hizi barabara zitakuwa zinapanuliwa na kupita, miundo misingi ya maji taka zitapita, usalama ama barabara zitakuwako, mashamba nayo yatakuwa yanaangaliwa kupewa title ili wajulikane wenyewe halisi ni kina nani. Kwa hivyo katika mfumo wote huu ambao Kamati imeweza kunukuu kipengele kimoja baada ya chengine wakigusia kila pembe ambayo ikipita itakapokuwa hii barabara ama itakapokuwa huu muundo msingi unaingia itakuwa inagusa, itaturahisishia hii kelele ya wananchi na kuona kuwa kwa nini sisi hatushuhuliwa kwa hivyo mimi ninaunga mkono Kamati hii kikamilifu na muzidi kuzingatia haya mambo mpaka yafanyike tuweze kuona Mombasa yetu imepata mabadiliko. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Hoja hii inaongelea haswa sehemu nne ambapo mradi wa KISIP ulienda ukaangazia na katika sehemu hizi nne, sehemu tatu zinatoka katika Wadi moja ambapo ni ya Mheshimiwa Mwamwiri wa Likoni na tunashukuru kwa sababu wakaazi wa hapo wakifaidika wakipata hati miliki itakuwa ni afueni maana leo ni huko na kesho itakuwa ni kwengine. Kwa hivyo hii hoja ni ya kusababisha na pia huu mradi si wa Kaunti pekee yake ni mashirika mengine ya serikali kuu, World Bank na pia Kaunti imeshirikiana ili wakaazi wa maeneo haya wapate hati miliki. Hivyo basi sisi kama wawakilishi wa wananchi pale nyanjani ninaamini ni furaha yetu kila mmoja wetu jambo kama hili kufanyika na pia tunaomba kwamba baada ya hii kumalizika, pia mradi huu wa KISIP ile raundi nyengine ikapate kuja na pia watu wapate kufaidi na pia nimemuona Mheshimiwa Frankline Makanga kutoka Chaani amesimama maana, Frankline Makanga watu wake walifaidi katika mradi wa awali na ninaelezwa kwamba ilikuwa iwe Mikindani lakini kukawa... ngoja kidogo wacha kuniangalia vibaya vibaya na hatukuwa katika Bunge hili ilikuwa ni ule muhula uliopita na kwa sababu ya

mshike mshike na watu bado kuleta siasa kule kule ndio ikapelekwa Chaani. Kwa hivyo huyu Mheshimiwa alifaidi na pia hawa wa leo wakifaidi tunashukuru Mungu maana pia wengine tutafaidi kesho. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes, Honourable Frankline?

Hon. Makanga: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza tushukuru kwa sababu tumerudi salama kutoka kwa likizo ila Mheshimiwa Spika niungane na wakatholiki wote kuweza kutoa rambirambi zangu kwa marehemu Papa ambae aliweza kutuacha jana kwa hivyo kwa kanisa la katoliki likiwa na wafuasi wengi zaidi wa Kanisa hilo, Mungu awape nguvu ya kuweza kuomboleza kiongozi wa kanisa hilo. Pili, Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa sababu ya Ripoti hii ambayo imeweza kuletwa na Kamati ya Mipangilio ya Mji ya Ujenzi na pia Maswala ya Ardhi. Mheshimiwa Spika, japo Mheshimiwa aliyenitangulia ambaye ni Askofu mpakwa mafuta wa Mungu ninaye muheshimu ameweza kusema mambo ambayo sina uhakika nayo na siwezi mtoa makosa kwa sababu ni askofu; lakini kungekuwa na nafasi ya yeye kuthibitisha ya kwamba mradi ule ulioletwa wadi ya Chaani na shirika la KISIP ulikuwa uende kwake basi tungefurahia ili inapoingia katika nukuu na kumbukumbu za Bunge hili tuwe tuna nukuu...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): There is an Honourable Member who is up, what is it Honourable Jactone Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa wa kutoka Wadi ya Chaani ambae ni rafiki yangu sana ambapo alisomea udaktari akamaliza, akaanza tena akasomea uwakili akamaliza na hivi sasa nasikia anaanza kusomea mambo ya *engineering*. Sasa sijui baada ya hapa anataka kuwa nini? Amesema nithibitishe! Mheshimiwa Spika Naibu Mwenyekiti yuko hapa na Kamati, namjibu Bwana Spika...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): I thought you are up on a point of order because...

[Interruption]

Hon. Madialo: Okay, sawa amesema nithibitishe ...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): If it was to, I was the one to tell you to rise and authenticate your sentiments; so please just sit let him proceed.

Hon. Madialo: Most obliged Sir, but I would love to authenticate...

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Okay, I will give you a chance...

[Interruption]

Hon. Madialo: Ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Proceed.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kweli nywele nyeupe hulinganishwa na hekima na ninavyoona Mheshimiwa Spika, Mungu amekujaalia kuanza kua na nywele nyeupe na hio inadhihirika katika uongozaji wako wa biashara za Bunge hili ndio maana kwa hekima yako umeweza kumketisha Askofu angoje ajuzwe na aambiwe yale yanayostahili kuendelea. Mheshimiwa Spika kama nilivyotangulia kusema ya kwamba yale mengi ambayo yamesemwa na tena akaongezea na uongo kwamba hivi sasa nimeanza tena kuendeleza masomo ya mambo na *Engineering*, hio si kweli, Askofu anafanya dhambi na dhambi zote zilifutwa hili juma kwa kufufuka kwa Yesu, kwa hivyo hilo sijui atasamehewa na nani? Mheshimiwa Spika tukirudi kwa Ripoti ambayo iko mbele yetu, kwanza niipongeze Kamati kwa sababu mradi huu ambao umependekezwa kufikia sasa ili uweze kufanyika maeneo ya Kibundani, ya Kikambala kwa mara ya kwanza ilikuwa nadhani labda nadhani ni kule kwa majirani ya Mheshimiwa Allen Katana lakini nasikia Kikambala hii iko Likoni kuna kwa Basra na Kidunguni. Mheshimiwa Spika miradi hii inapokuja kwa jamii, inaweza kuleta natija na maendeleo ambayo Mheshimiwa Spika hayana kifani. Mimi nikiwa shahidi ni kwamba nilipochaguliwa tarehe 9/8/2022 kufikia saa mbili usiku nikawa nimeshinda kuwa mwakilishi wadi wa Chaani, Mheshimiwa Spika nilitia nia kufwatilia kujua kila KISIP mradi ambao ulikuwa umeanza na ukawa umekwama kwa miaka kiasi, ni nini ilifanyika? Na kufwatilia huko Mheshimiwa Spika iingie katika kumbukumbu tuliweza kupata suluhu na tunavyoongea Mheshimiwa Spika wananchi wa Chaani, maeneo ya Mwatate na kwa Rasi wameweza kupata hati miliki beneficiaries karibu 600 Mheshimiwa Spika, ingekua wenzangu hapa hawana wivu nafikiri kwa sasa wangekuwa wamenipigia makofi...

[Applause]

Upande huu wana wivu Mheshimiwa Spika lakini tutawaombea. Mheshimiwa Spika, katika maeneo hayo hayo tumeona kumekuwa *up grading* ya mitaro ya maji; mahali ambapo pia hakukuwa na barabara kumeweza kutengezwa barabara na wale ambao walikuwa wamejenga katika barabara hizo wakafidiwa inavyostahili. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika maendeleo haya kama yatakuja katika jamii yetu ya wana Likoni na pia kipindi chengine iweze kwenda kama ni maeneo ya Wadi ya Jomvu haswa maeneo ya Bangladeshi ambapo Mheshimiwa Jactone Madialo anatoka nina amini tukiweza kuwatia moyo mashirika haya kushirikiana na serikali basi tutaweza kuendeleza mji wetu na tutaendelea kuona manufaa. Kwa hivyo mimi Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono na kuunga Mkono Mwenyekiti wa Kamati hii Ndugu Ahmed Khamis kuhakikisha ya kwamba ripoti hii inaweza kupitishwa na Bunge hili na iweze ianze kufanyiwa kazi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika nasimama kuunga mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you Honourable Frankline. Honourable Members, just a minute there is an Honourable Member who was mentioned though indirectly, Honourable Frankline Makanga, used the name *Askofu*. I think you were directing to Honourable Madialo, so Honourable Honourable Madialo please reply and prove to this Honourable House that the previous regime used the back door to remove KICIP from Mikindani to his Ward!

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 6*

Just one minute because you had already debated on this Motion.

Hon. Madialo: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kamati ya Ardhi ilikutana na Wizara ya Ardhi na siku hio pia kwa sababu Mheshimiwa Mwamwiri pia amehusika maana hizi tatu zinaenda kwake pia alialikwa. Sasa walivyokuwa wakiendelea kuelezea mimi nikauliza swali kuhusu Mikindani kwa sababu, najua na huyu anajua hapo mahali panaitwa Jitengeni. Jitengeni kuliwa na program ya KICIP lakini ikakwama, nikauliza kwa nini imekwama? *Director* wa Ardhi Madam Rose akanijibu ya kwamba, Mikindani kulingia siasa kuhusu hio mashamba na ndiposa ikapelekwa Chaani, na sijasema kwa ubaya maana Chaani pia watu wakifaidika huko ni sawa na sikuweko mimi kama MCA wakati huo uliopita. Sasa mimi ndio MCA sasa, kukitokezea chance nyengine ya Mikindani tutaichukua ahsante.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. Yes Katana Allen?

Hon. Katana: Let me thank you Honourable Speaker for this wonderful moment that you have also given me, at least so that I can air out my few points in this. Honourable Speaker, I really want to appreciate the work that our Committee and I am saying ours, because I am also a Member of this Committee under the leadership our very able Deputy Chair. Mr. Speaker, as it has been said by many Honourable Members that, whatever this Motion is bringing, it is equally beneficial to our people and I also truly want to support this Motion but also with the reservation Mr. Speaker being, I consider myself as a very active Member of this Honourable Committee and I stand to support, but as I have said with reservation and the reason being is, I do not know any of these places. Like it has been said by *Daktari* here that he thought Kikambala was in Kilifi County but, only to understand that Kikambala is also in Mombasa County. I know very well of Kibundani but it is in Ukunda. It is my humble request and submission that or maybe when it was done I was not in that particular trip or meeting, but my humble request and submission is that, whenever we have such a Motion that will come to this Honourable House, it is very good and I guess it is the best practice that this very Committee to visit these places, because whatever goodies come they also come with some other things that maybe will harm our people and all sought of things and Mr. Speaker, let me not speak much but I also stand to support this Motion thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Thank you. I will now let the mover of the motion to reply Honourable Ahmed Khamis.

Hon. Ahmed Khamis: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nimesimama hapa kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu kwa kuunga hii hoja na haswa watu ambao wanahusika zaidi na huu mradi ambao utawanufaisha watu wa eneo lao, naomba muiunge mkono ili waeze kufaidika ahsanteni sana.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Makarani): Honourable Members, I now stand to put a question that the Motion as moved by Honourable Ahmed Khamis on the Draft Report on Local Physical and Land Use Development Plan for Kikambala, Kisimani, Kwa Ndegwa, Kidunguni, Kibundani and Basra Informal Settlements 2024 to 2034 be approved by this Honourable House.

[Question put and agreed to]

Honourable Members, the Motion has been approved by this Honourable House.

ADJOURNMENT

Honourable Members, the House stands adjourned until today afternoon 22nd April at 2:30p.m.

The House rose at 11:58 a.m.